

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA



Simu: +255 686 397 972
+255 754 422 746

S.L.P 72,
KYERWA.

Nukushi:
Barua : : ded@kyerwadc.go.tz

Kumb. Na. BC.253/517/8/39

24/04/2018.

TANGAZO MWONGOZO KWA WAFUGAJI WA MBWA WILAYANI KYERWA

Kumekuwa na wimbi la mbwa wanaozurura na wasiotunzwa na wamiliki wa mbwa hao kwenye maeneo mbalimbali Wilayani Kyerwa. Hii ni kinyume na ***Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya Mwaka 2008 Sehemu III Kifungu cha 16(1) na Kifungu 57(1) na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya Mwaka 2003.***

Kwa mujibu wa Sheria hizo, kila mfugaji wa mbwa anatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

- (i) Kuhakikisha kuwa anafunga mbwa wake saa 11.30 asubuhi na kumfungua saa 4.00 Usiku.
- (ii) Kuhakikisha kuwa mbwa anajengewa banda bora la kumtunzia/kumfugua wakati wote wa mchana na awe na mnyororo madhubuti.
- (iii) Endapo mbwa anasafirishwa kutoka sehemu/eneo moja kwenda eneo lingine, lazima awe amefungwa kwa mnyororo madhubuti.


- (iv) Mbwa wapatie chakula cha kutosha na wakingwe dhidi ya vimelea vya magonjwa.
- (v) ***Kuhakikisha kuwa mbwa wake anachanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa kila mwaka bila kukosa.***
- (vi) Kuweka kibao/bango linalotoa tahadhari kwa wananchi kuwa kuna mbwa mkali kwenye eneo husika.
- (vii) Kutoa taarifa kwa mganga wa mifugo wa Kata, pindi mbwa anapoonesha mabadiliko ya tabia ili kupata huduma stahiki na kuchukua tahadhari.
- (viii) Kutoa taarifa kwa Mganga wa Mifugo wa Kata pindi mbwa wake anapokufa, kuuzwa au kumilikiwa na mfugaji mwingine.
- (ix) Kila mfugaji wa mbwa anaponunua/kuingiza mbwa mgeni inabidi ***kusajili mbwa*** huyo kwa mganga wa mifugo wa Kata.

Wafugaji ambao hawatazingatia Mwongozo huu ***watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria*** zinazosimamia utunzaji/ufugaji bora wa mbwa.

Ndugu Wananchi,

mnaombwa kutoa ushirikiano pindi mtakapobaini wafugaji wa mbwa ambao hawafungi mbwa wao na au makundi ya mbwa wanaozurura kwenye maeneo yenu.. Taarifa itolewe kwa **Mtendaji wa Kijiji** husika na **Mganga wa Mifugo Kata.**

Nawatakia utekelezaji Mwema


Prosper Rutakinikwa
AFISA MIFUGO (W)

HALMASHAURI YA WILAYA KYERWA

**AFISA MIFUGO NA UVUVI
WILAYA - KYERWA**